**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**

**Namba za Simu:**
Mkuu wa Shule: 0754 092 668
Makamu Mkuu wa Shule: 0623 579 292
Patron: 0753 659 635

Shule ya Sekondari Ihungo,
S.L.P. 95,
**Bukoba.**
Tarehe: ………………

Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi
……………………………………………..
S.L.P. ……………………………………
……………………………………………..

Yah:-**MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI IHUNGO -HALMASHAURI YA BUKOBA (M) MKOA WA KAGERA- MWAKA 2022**

1. Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii Mwaka 2022 kwa tahasusi ya………….. Shule ya Sekondari IHUNGO ipo umbali wa Kilometa 04 Kaskazini mwa Mji wa Bukoba. Kutoka mjini kwenye vituo vya Taxi/Bus Stand gharama si zaidi ya TSh. 10,000/= kwa usafiri wa Taxi. Pia usafiri wa Pikipiki unapatikana si zaidi ya Shs.1,500/- kutoka Bukoba Mjini.

   Muhula wa masomo unaanza tarehe **…………….** Hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe **………………**. Mwisho wa kuripoti ni tarehe **……………….**

2. **Mambo muhimu ya kuzingatia**:
   2.1: Sare ya Shule:
   - a) Aje na Suruali mbili nyeusi zenye marinda mawili kila upande, mifuko 2 ya kawaida pembeni, mfuko 1 nyuma wenye kifungo na pindo la chini (turn-up). Mapana kwa chini (yaani miguuni) iwe na vipimo vya inchi 16 – 18 .(zisiwe za mitumba).
   - b) Aje na Mashati mawili meupe ya mikono mifupi (Tetron) – yasiwe ya mitumba.
   - c) Aje na jozi mbili za Viatu vyeusi vya ngozi vya kufunga na kamba (visivyochongoka visiwe na sorindefu/kubwa sana) na soksi Nyeusi/dark blue) jozi mbili au zaidi.
   - d) Aje na Mkanda mweusi wa ngozi wa suruali, usiwe na Bi-ross pana wala wenye maandishi au picha yoyote.
   - e) Aje na sweta moja ya rangi ya Kijivu kizito (Deep grey) yenye shingo duara nyuma na V mbele
   - f) Aje na T-Shirt mbili za rangi ya Light Blue zenye nembo ya shule nyuma mgongoni, ziwe nzito na zisiwe na kola.(**T – Shirt zisizo na nembo ya shule hazitapokelewa).**
   - g) Aje naTai moja ya rangi ya Light Grey yenye michirizi mieupe ya kukatiza kwa mshazari.
   - h) Aje na suruali za kitambaa mbili rangi ya “dark-blue” kwa ajili ya kushindia (sifa ya suruali hizi iwe sawa na kifungu (a) hapo juu.
   - i) Aje na nguo za michezo (Bukta, T- Shirt na soksi) za ***Kampuni ya ADIDAS*/SPORTS (T – Shirt isiwe na maandishi yoyote tofauti na nembo ya Kampuni),** pamoja na raba za michezo**Vitavaliwa wakati wa michezo uwanjani tu.** Rangi ya Bukta, T – Shirt na soksi inatokana na tahasusi uliyopangiwa kwa mchanganuo ufuatao:-
     ***HGE – Blue, EGM – Rangi ya machungwa, CBG – Nyeusi, PCM – Kijani na PCB – Nyekundu.***

***NB: Kwa mzazi yeyote atakayepata mkanganyiko juu ya sare zilizotajwa apige simu kati ya namba zilizoorodheshwa ili kupata maelekezo zaidi kabla ya manunuzi ili kuondoa kununua sare isiyo sahihi.***

***Mwanafunzi hatakiwi kuja na Shati, Suruali au nguo nyingine zozote tofauti na hizo alizoagizwa. (HAZIRUHUSIWI KABISA SHULENI).***

2.2: **Ada na Michango ya Shule**

a) Ada ya Shule kwa mwaka ni Shilingi 70,000/- kwa mwanafunzi wa Bweni. Mwanafunzi wa Bweni anaweza kulipa kiasi cha Shilingi35,000/- kwa muhula au kulipa ada yote kwa mara moja. Fedha hizo zilipwe kwenye Akaunti ya Shule Na. **31801000020** katika Benki ya NMByenye jina Ihungo Secondary School. (***Tafadhali andika jina la mwanafunzi kwenye pay in slipna kuja nayo shuleni).***

b) Michango inayotakiwa kulipwa na kila mzazi ni:

i. Shilingi 15,000/- kwa ajili ya ukarabati wa samani.
ii. Shilingi 6,000/- kwa ajili ya kitambulisho na picha
iii. Shilingi 20,000/- kwa ajili ya taaluma
iv. Shilingi 30,000/- kwa ajili ya kuwalipa wapishi, walinzi na vibarua wengine.
v. Shilingi 2,000/- kwa ajili ya nembo ya shule kwenye mashati mawili.
vi. Shilingi 10,000/- kwa ajili ya huduma ya kwanza.
vii. Fedha ya tahadhari TShs.5,000/- (haitarejeshwa).

**Ada pamoja na michango mengine ya shule kama ilivyoorodheshwa hapo juu ilipwe kwenye Akaunti ya Shule namba 31801000020 katika Benki ya NMB yenye jina Ihungo Secondary School.** (***Tafadhali andika jina la mwanafunzi kwenye pay in slip na kuja nayo shuleni).***

c) **Mahitaji muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuleta shuleni ni:-**

i. Ream ya karatasi nyeupe (A4) 1(moja) pamoja na Ream ya karatasi za mistari moja.
ii. Graph Pad 1( moja) yenye karatasi hamsini.
iii. Ndoo mbili ndogo zenye mifuniko.
iv. Kwanja 1(lililonolewa), jembe 1, reki 1, mfagio laini wa plastiki (soft broom) mmoja , mfagio mgumu wa plastiki (hard broom) mmoja, mfagio wa nje(chelewa)mmoja, kotama 1na mopper/flap
v. Vitabu vya masomo ( tahasusi) anayochukua. (Angalia kiambatisho D).
vi. Dissecting kit kwa wanafunzi wa Biolojia
vii. Scientific calculator – non programmable.
viii Aje na stop watch (digital) kama anachukua tahasusi ya Sayansi.
ix. Godoro 1 la sponge size Futi 2 na nusu kwa sita (2½' x 6')
x. Mashuka 2 rangi ya Pinki, Blanketi 1, Mto na foronya ya pink, chandarua 1
xi. Vyombo vya chakula (Sahani, bakuli, kijiko na Kikombe)
xii. Vitambaa vya mkononi. Uje na vitambaa 2 vyeupe au zaidi.
xiii. Kandambili, Taulo, Fulana 2 nyeupe (Vest), Chupi 2 au zaidi.
xiv. "Toilet Papers" za kutosha.
xv. Vifaa vya Darasani: Kalamu za wino na risasi, kifutio, rula, madaftari na mkebe wa vifaa vya Hesabu (Mathematical Instruments) bila kusahau Kamusi ya Kiingereza.

**NB:** Kwa wanaotoka mbali na watakaopenda baadhi ya**vifaa vyataaluma (**Ream, daftari, graph pad, Dissecting kit, Scientific calculator, n.k**) na vifaa vya usafi (**Kwanja ,jembe, reki, soft broom ,hard broom , mfagio wa nje (chelewa), kotama, Ndoo na flap) pamoja na **vyombo vya chakulavitapatikana kwenye duka la shule kwa bei ya kawaida. Wasiliana na namba zilizotajwa.**

3. **KUFIKA SHULENI/ SIKU YA KURIPOTI SHULENI**

- Mwanafunzi anatakiwa kufika hapa shuleni tarehe …………… saa 3:00 asubuhi. Mara afikapo shuleni aripoti mara moja Ofisini kwa Mkuu wa Shule akiwa na mahitaji yote ya Shule aliyojulishwa hapo juu tayari kwa kukaguliwa. Akichelewa kuripoti zaidi ya wiki mbili bila sababu maalum baada ya shule kufunguliwa atapoteza nafasi yake.
- Siku za kuripoti ni Jumatatu hadi Ijumaa kuanzia saa 2.00 asubuhi hadi saa 9.30 Alasiri (muda wa kazi).
- **Kila mwanafunzi aje amevaa suruali nyeusi na shati jeupe la mikono mifupi (sare ya shule).**

Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**TANIBIHI:**

1. Ili kuepukana na usumbufu wa kurudishwa nyumbani kutokana na kutotimiza mahitaji, unashauriwa kukamilisha mahitaji haya kabla ya kuripoti shuleni.
2. **Lazima aje na bima ya afya ya mwanafunzi inayotolewa na NHIF (Shirika la Taifa la Bima ya Afya) kwa gharama ya Tsh. 50,400/- tu.**
3. CHETI KUTOKA KWA DAKTARI: Itamubidi arudishe fomu iliyoambatishwa ikiwa imethibitishwa na Daktari wa Hospitali ya Serikali ya Halmashauri ya Wilaya au ya Mkoa kuwa umepimwa na kwamba anaweza kumudu masomo na kazi za nje bila matatizo.
4. Aje na RESULT SLIP yake ya Kidato cha Nne. (Original na Copy moja).
5. URAIA: Anatakiwa kuleta shuleni Copy moja ya CHETI CHA KUZALIWA (Birth Certificate)
6. KUKUBALI MASHARTI YA SHULE: Sheria za Shule na Fomu ya kukubali kutii kidhati Sheria hizo pamoja na fomu ya maelezo yako binafsi vimeambatanishwa. Mwanafunzi azisome kwa makini Sheria hizo, akizikubali, aweke saini yake kwenye fomu ya kukubali kujiunga mbele yako mzazi au mlezi, pia ajaze fomu ya maelezo binafsi ya mwanafunzi naaziwasilishe fomu hizo shuleni siku ya kuripoti.
7. Abandike Picha nne (4) za wazazi au ndugu wa karibu pamoja na namba zao za simu wanaoweza kumtembelea mwanafunzi na kushirikiana na shule katika malezi.
8. USAFIRI: Itamubidi ajigharimie kwa usafiri wa kuja shuleni na kurudi nyumbani wakati wa likizo.

4. Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII.**

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI IHUNGO
S.L.P 95
BUKOBA

**OFISI YA RAIS TAMISEMI**
**HALMASHAURI YA MANISPAA BUKOBA**
**SHULE YA SEKONDARI IHUNGO**
**SHERIA NA KANUNI ZA SHULE**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa **sheria ya Elimu Na.25 ya mwaka 1978**. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara yenye dhamana ya Elimu Nchini. Unatakiwa kuzingatia kanuni na sheria hizi kwa kipindi chote utakachokuwa hapa.(Maelekezo mengine utapewa mara ufikapo shuleni.

1. Kila mwanafunzi ni lazima kuvaa nguo rasmi za shule (School Uniform), wakati wote awapo shuleni, na mahali pengine atakapotakiwa kufanya hivyo.
2. Ni muhimu na wajibu kwa kila mwanafunzi kuwahi bila kuchelewa mahali popote utakapohitajika darasani, kazini, mstarini nk.
3. Juhudi katika kazi za mikono, madarasani na katika michezo ni wajibu wa kila mwanafunzi. Uzembe katika shughuli hizi hauruhusiwi kabisa.
4. Kila mwanafunzi wa shule hii ni lazima aombe ruhusa endapo atakosa kuwapo shuleni. Hata hivyo mwanafunzi atalazimaka kurudi shule kabla ya saa 11.50 jioni kila inapotokea kuwa nje ya shule kwa sababu yoyote ile.
5. Kila mwanafunzi ni wajibu kujiheshimu yeye binafsi na kuwaheshimu watu wengine kama anavyopenda kuheshimiwa.
6. Ni wajibu wa kila mwanafunzi kutunza na kulinda siha na usafi wake binafsi (Usifuge ndevu, nywele ndefu, kucha n.k) na wa mazingira yote ya shule nje na ndani ya madarasa, vyoo n.k.
7. Vitendo vyovyote vya kushiriki au kushawishi mgomo wa aina yoyote shuleni ni marufuku kabisa.
8. Ugomvi au kupigana, kuleta fujo madarasani, lugha za matusi,kashfa kwa wenzako au wananchi ni mwiko kabisa.
9. Vipindi vyote vilivyoko kwenye ratiba ni lazima uvihudhurie bila kukosa pamoja na shughuli za nje ya darasa.
10. Kila mwanafunzi sharti aepuke na kuchukia vitendo vyovyote vya uongo, uzushi,wizi, uasherati, ulevi, uvutaji sigara na uchoyo.
11. Upole na utii kwa viongozi ni wajibu kwa kila mwanafunzi; Ubishi wenye lengo la kukwepa kutimiza wajibu ni marufuku kabisa!
12. Makoti,vibandiko,vizibao, kofia,kandambili,viatu vya wazi,mikanda mipana haviruhusiwi kamwe kuvaliwa wakati mwanafunzi awapo ndani ya vazi la shule
13. Lugha inayotumika hapa Shuleni ni Kiingereza tu.
14. Kutimiza kwa makini maandalizi ya jioni (Preparation).
15. Ni marufuku kuwa na**SIMU ya Mkononi** (Mobile Phone), Chip (line), Earphone/Headphone, charger, Powerbank, kompyuta (Laptop), I pad, pasi ya umeme, heater za umeme, Redio, Kondomu n.k. **USIJE NAVYO SHULENI.**
16. Ni marufuku kupeleka chakula mabwenini.
17. Ni marufuku kumiliki kifaa chochote kinachoweza kusaidia kufanya biashara shuleni au kufanya biashara yoyote mwanafunzi awapo shuleni. Mfano: Kamera, kuuza vyakula au vinywaji n.k.
18. **Makosa yafuatayo yaweza kukufanya ufukuzwe ama kutolewa shuleni:-**

a) Wizi
b) Ulevi au unywaji wa pombe, uvutaji wa sigira na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli n.k.
c) Ubakaji
d) Kudharau bendera ya Taifa
e) Kuoa au kuolewa
f) Uharibifu wa makusudi wa mali ya umma
g) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa shule.
h) Kukataa adhabu kwa makusudi
i) Kupigana au kupiga
j) Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/Utoro wa masomo.
k) Kushawishi/kushiriki katika migomo
l) Kutofanya mitihani na mazoezi
m) Mapenzi ya ngono na wanafunzi wenzako shuleni au watu wengine nje ya shule(Uasherati na ushoga)
n) Kumpa mimba mwanafunzi wa kike.
o) Mwanafunzi kuwa na **SIMUya Mkononi** au kifaa chochote kinachohusiana na simu.
p) Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi.
q) Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni.
r) Kufanya jaribio lolote la kujiua au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k.
s) Kupanga/kuishi mitaani ukiwa shuleni/wakati wa masomo.
t) Kutenda tendo lolote lisilokuwa la kawaida shuleni au nje ya shule.

**MASHARTI MENGINE**

Mwanafunzi akifanya uharibufu wa makusudi au kwa uzembe katika miundombinu iliyoainishwa hapo chini atawajibika kurejesha miundombinu hiyo katika hali yake ya kawaida pamoja na hatua zingine za kinidhamu.

- Uharibifu wa miundombinu ya umeme. Mfano: kuchubua nyaya za umeme ili kuchaji simu, kuchemsha maji/chai n.k.
- Uharibifu wa miundombinu ya maji Mfano: kuharibu tepu za bomba la maji, n.k.
- Uharibifu wa miundombinu ya majengo. Mfano: kupasua vioo, kuchafua kuta, kuharibu vigae, n.k.
- Uharibifu wa miundombinu ya vyoo. Mfano: kuweka vitu vigumu (mawe, vipande vya magodoro, karatasi, nguo n.k) kwenye matundu ya vyoo vya maji.

**NB: Mwanafunzi atakayepoteza kifaa chochote cha shule kwa uzembe au makusudi mengine na akabainika atatakiwa kununua kifaa kingine cha aina hiyo hiyo ili kufidia upotevu huo.**

**KIAMBATISHO A**

Anwani ……………………………………
…………………………………………….
……………………………………………
……………………………………………
Tarehe……………………………

Mkuu wa Shule,
Shule ya Sekondari Ihungo,
S.L.P. 95,
Bukoba.

**YAH:-KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI IHUNGO**

Mimi……………………………………………………………*(Jina la Mwanafunzi)* nimepokea barua ya kuchaguliwa kujiunga na **Kidato cha TANO** katika Shule ya Sekondari Ihungo kuanzia mwaka……… *_**Nakubali/Sikubali**_ nafasi hiyo. **Nimesoma na kuelewa Sheria na masharti ya kujiunga na shule hii yaliyoambatanishwa.** Hivyo ninaahidi kujifunza kadri ya uwezo wangu wote bila kupoteza muda au kufanya mzaha wowote kama Sheria zilivyo ainishwa. Nitatimiza wajibu wangu wote kwa muda na wakati uliopangwa. Pia ninaahidi kuwa nitatii sheria zote za shule.**Endapo nitashindwa kutii na kufuata sheria hizo hatua zinazostahili zichukuliwe dhidi yangu.** Natoa ahadi hizi mbele ya Mzazi/Mlezi wangu, ambaye naye ametia sahihi yake kwenye kifungu kinachofuata hapa chini.

……………………………………………..　　　　　　　　……………………….
**SAHIHI YA MWANAFUNZI**　　　　　　　　**TAREHE**

Mimi……………………………………………………(jina la **Mzazi/Mlezi*)
*Nakubali/Sikubali mtoto wangu ajiunge na Shule ya Sekondari Ihungo. Nimesoma na kuelewa sheria na masharti ya kujiunga na Shule hii. Hivyo nakubaliana na masharti na sheria hizi ambazo itambidi mwanangu azifuate kama alivyoahidi mbele yangu. Nipo tayari kulipa Ada na michango yote. Nitashirikiana na uongozi wa shule pamoja na jumuiya nzima ya shule katika kutoa malezi bora kwa mwanangu kulingana na sheria za shule na matakwa ya Taifa kwa ujumla.
Taarifa na mawasiliano yote yahusuyo mwanangu yatumwe kwangu kwa kutumia anwani ifuatayo:
…………………………………………………….
…………………………………………………….
…………………………………………………….
……………………………………………………. Namba za simu:……………………………
……………………………………
……………………………………
Mabadiliko yoyote ya anwani yangu nitayatuma kwa Mkuu wa Shule kwa maandishi.

Sahihi ya **Mzazi/Mlezi* ………………………………　　　　Tarehe…………………………..

***Futa isiyotakiwa***

**KIAMBATISHO B**
**MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI**

1. Jina kamili ………………………………………..…………………………………………
   *(kama lilivyo kwenye Form four SEL Form na Birth Certificate)*
2. Tarehe ya kuzaliwa…………………………………………………………………………..
3. Anwani ya nyumbani……………………………………………………………………….
   Mahali unapoishi (Nyumbani kwenu): Wilaya……………………Tarafa…………………….
   Kata…………………………. Kijiji………………………………
4. Shule ya Sekondari ulikotoka……………………………………………………………….

   Anwani…………………………………………………………………………………………
   ………………………………………………………………………………………………
5. Dini…………………………………..
6. Kabila………………………………..
7. Taifa (*Mtanzania/si Mtanzania)* ……………………………………….
8. Jamaa katika familia: (*Watakaohusishwa katika malezi ya mwanafunzi akiwa hapa shuleni)*

   i. Jina la Baba……………………………………………………..
      Anwani…………………………………………………SIMU NA. 1………………
      Anaishi/Haishi…………………………………………… 2. ………………
      Kazi yake…………………………………………………

      | Picha ya Baba mzazi |
      |---|

   ii. Jina la Mama…………………………………………………..
       Anwani…………………………………………………SIMU NA. 1. ………………
       Anaishi/Haishi…………………………………………… 2………………
       Kazi yake…………………………………………………

       | Picha ya Mama mzazi |
       |---|

   iii. Jina la Mlezi……………………………………………………
        Anwani……………………………………………………..SIMU NA.1. ………………
        ………………………………………………………… 2………………
        Kazi yake ………………………………………………..
        Uhusiano wake na wewe…………………………………

        | Picha ya Mlezi / Ndg. wa karibu |
        |---|

   iv. Jina la Mlezi……………………………………………………
       Anwani……………………………………………………..SIMU NA. 1. ………………
       ………………………………………………………… 2………………
       Kazi yake ………………………………………………..
       Uhusiano wake na wewe…………………………………

       | Picha ya Mlezi/ Ndg. wa karibu |
       |---|

   v. Idadi ya Kaka …………………………………………………….
   vi. Idadi ya Dada……………………………………………………..
   vii. Wewe ni wa ngapi katika familia…………………………………

Mimi ……………………………………………(*mwanafunzi)* nathibitisha kuwa taarifa nilizozijaza hapo juu ni za kweli.

……………………………… …………………………
Sahihi ya Mwanafunzi Tarehe

Mimi…………………………………….(*Mzazi/Mlezi)* wa mwanafunzi……………………………...
…………………………………nimehakikisha kuwa taarifa zilizojazwa hapo juu ni za kweli.

………………………………….. …………………………
Sahihi ya Mzazi/Mlezi Tarehe

*****Jina la Afisa Mtendaji wa Kijiji/Mtaa…………………………………………………………………
Sahihi ya Afisa Mtendaji wa Kijiji/Mtaa……………………………. Tarehe…………………………
Simu Na.: 1…………………….. 2. ……………………. 3. ………………………

**KIAMBATISHO C**
**BUKOBA MUNICIPAL COUNCIL**

Ihungo secondary School,
P.O..Box 95,
Bukoba.

Date…………………………

To Medical Officer,
……………………………………………
……………………………………………
……………………………………………
……………………………………………

**Ref:……………………………………………….(*Name of student)***

Please examine the above named student as per Medical examination form below:

……………………………..
**HEADMASTER**

MEDICAL EXAMINATION FORM
**(*To be completed by Government Medical Officer)***

Full Name……………………………………………………………………….
Age………………………… Height………………(cm) Weight……………(Kg)
1. Blood count……………………………………………………
2. Stool Examination…………………………………………….
3. Urinary………………………………………………………..
4. STDs and other V.D………………………………………….
5. T.B. and Leprosy test…………………………………………
6. Eye Test………………………………………………………
7. Ear Test………………………………………………………
8. Chest…………………………………………………………
9. Abdomen…………………………………………………….
10. Spleen………………………………………………………..

Any additional information:
E.g. Physical defects or impairments, infections, chronic or family diseases (eg.Sickle cell), in ability to eat certain foods etc.
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………
I have examined the above named student and I certify that he/she is ***FIT/NOT FIT*** to pursue Secondary Education.

……………………………………… ……………………….
Signature and Official Stamp Date

Station………………………………… Designation……………………

**KIAMBATISHO D**

**ORODHA YA VIBATU KWA KILA TAHASUSI**

Mzazi unashauriwa kumnunulia mtoto wako vitabu kwa kila somo analokuja kusoma kama ilivyoainishwa hapa chini.

**BIOLOGY**

i. Biology Science by DJ Tylot
ii. Understanding Biology for Advanced level by Grenn & Susan
iii. Advanced Biology Principles and Application by C.J.clegga and DG Mackean

**CHEMISTRY**

i. Inorganic chemistry by TIE (Part 1 & 2)
ii. Physical chemistry Vol I and II
iii. Physical chemistry by Chand
iv. Organic Chemistry by TIE

**PHYSICS**

i. Advanced Physics 7th Edition by Nelcon & Parker
ii. A level Physics by Rodgers Mancaster
iii. Essential Principles of Physics 2nd Edition by Whelang Hagson

**ECONOMICS**

i. Economics Simplified by N.A. Saleem
ii. Modern Economics by Robert Mudida
iii. Modern Micro Economics by Chand S
iv. Principle of Economics by M.L. Jinghan
v. Advanced Economy Book 1 & 2 Ambilikile C( 2009),
vi. Model questions and answers in economics Tayebwa BMB (2004)

**GEOGRAPHY**

i. Fundamental Geography By Josephat Mwita A.M
ii. Physical Geography By Monk House
iii. Practical Geography For Africa By John Richard

**ADVANCED MATHS**

i. Advanced level pure Math Vol I & II By J.K Backhouse
ii. S. Chand's Mathematics for class XI by H.K OASS, Dr. RAMA VERMA
iii. Advanced mathematics form V & Form VI by S.I. Sillem

**HISTORY**

i. Advanced level History for form Five and Six by Oxford
ii. Advanced level History paper 1&2 by Z. Kamili
iii. The Evolving world by Denis Ngalula

- Kila mwanafunzi anatakiwa kuwa na kitabu cha somo la General studies (Understanding Advanced, General Studies by J.Bigirwamungu & Sospeter)

- Kwa wanafunzi wanaosoma CBG, PCB na HGE kila mmoja anatakiwa kuja na kitabu cha somo la Basic Applied Mathematics (Basic Applied Mathematics by MAT)